## Dkt. Samia ataka umeme wa kujitosheleza nchini

NA MWANDISHI WETU

NIA ya Rais wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan ni kuona nchi inajitoshelaza kwa nishati ya umeme, ambapo dhamira

Inaendela -Uk. 2



## Mkurugenzi azindua Kitabu malezi ya watoto

NA HUSNA NASSORO

MWANDISHI wa kitabu cha Elimu na Malezi kwa Watoto Katika Zama za Kidijitali ambaye pi ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya

Inaendela -Uk. 4

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

# Tanzania BORA

Ni Mimi na Wewe

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz | ISSN 4256-1873 Toleo Na.12 Tanzania Bora Jumanne Januari 28, 2025 Bei Tsh. 1,000

## Dkt. Samia aridhishwa na maendeleo mji wa Kibaha

HABARI UK. 4

# Wajumbe mkutano wa nishati Wafagilia maendeleo Tanzania




NA MWANDISHI WETU

VIONGOZI mbalimbali waliowasili katika Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa Nishati Afrika, wameeleza kuvutiwa na maandeleo ya nchi ya Tanzania yanayozidi kuimarika kila siku.

Tanzania imepokea zaidi ya Marais 25 na Mawaziri 60, katika mkutano huo ulioanza jana ambao unatarajiwa kumalizika leo, huku ajenda ikiwa ni kushirikiana kwa pamoja ili kuimarisha juhudi za kukabiliana na changamoto za nishati Barani Afrika.

Katika mkutano huo pia alihudhuria Rais wa Nigeria Bola Ahmed Tinubu aliyewasili na kupokelewa na Waziri wa Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Mahmoud Thabit Kombo.

Inaendela -Uk. 2

## 'Chadema inaogopa Kivuli chake

NA ALBANO MIDELO, **Mbinga**

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma, umetenga zaidi ya shilingi milioni 468 kwa ajili ya kuendeleza mradi wa ujenzi wa Barabara ya Kihamili–Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwa kiwango cha lami.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Mbinga, Oscar Mussa, amesema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 3.4 inajengwa kwa awamu, ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imejengwa kwa kiwango cha lami urefu wa mita 750.

Inaendela -Uk. 3

# CCM Dar wasema mitano kwa Dkt. Samia ipo palepale

SOMA UK. 2

# Wajumbe mkutano wa nishati wafagilia maendeleo Tanzania

NA MWANDISHI WETU

VIONGOZI mbalimbali waliowasili katika Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa Nishati Afrika, wameeleza kuvutiwa na maandeleo ya nchi ya Tanzania yanayozidi kuimarika kila siku.

Tanzania imepokea zaidi ya Marais 25 na Mawaziri 60, katika mkutano huo ulioanza jana ambao unatarajiwa kumalizika leo, huku ajenda ikiwa ni kushirikiana kwa pamoja ili kuimarisha juhudi za kukabiliana na changamoto za nishati Barani Afrika.

Katika mkutano huo pia alihudhuria Rais wa Nigeria Bola Ahmed Tinubu aliyewasili na kupokelewa na Waziri wa Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Mahmoud Thabit Kombo.

Katika mazungumzo yao pamoja na mambo mengine alisifu juhudi kubwa za maendeleo ya Tanzania katika kipindi hiki cha uongozi wa Awamu ya sita chini ya Dkt Samia Suluhu Hassan.

Kulingana na wajumbe waliohudhuria mkutano huo mambo ya kuvutia yanayotajwa na wageni wengi ni kuwepo na utulivu na amani, pia masuala ya utalii ambayo kwa sasa yamepiga hatua kubwa hapa nchini.

Kuna matarajio makubwa baada ya msafara huu kurejea katika nchi zao, Tanzania itaanza kupokea watalii wengi watakaopata taarifa njema kutoka kwa wageni hawa waliokuwepo nchini kwa siku mbili za mkutano huo.

Kwa upande mwingine Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko amesema kuwa Tanzania inachukulia mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika (Misheni 300) kuwa ni kichocheo cha utekelezaji wa Sera yake ya Taifa ya Nishati ya kuendeleza nishati na uhifadhi.

Dk Biteko aliwaambia wajumbe wa mkutano huo jana Januari 27, 2025 wakati akifungua Mkutano huo unaofanyika Ukumbi wa Mwalimu Nyerere Jijini Dar es Salaam kwa siku mbili, kuanzia leo Januari 27 hadi 28, 2025 ambapo majadiliano ya leo yamehusisha ngazi ya ukijumuisha Mawaziri na Wadau wa Nishati na Fedha na kesho mkutano huo utahusisha ngazi ya viongozi wakuu wa nchi za Afrika.

Alisema maendeleo ya nishati tunayojivunia, bado nchi inahitaji uwekezaji zaidi katika sekta ya nishati kwani matarajio yake ni kukuza shughuli za kiuchumi hususan katika sekta za viwanda, madini na huduma za ukarimu jambo ambalo linahitaji uwekezaji wa kimkakati zaidi katika sekta ya nishati.

# Chadema inaogopa kivuli chake

NA MWANDISHI WETU

CHAMA Cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA kimetakiwa kuacha kuhangaika na CCM badala yake wapambane kurudisha nidhamu katika Chama chao.

Hayo yamesemwa na wanachama na wapenzi wa CCM waliozungumza na gazeti hili katika mkutano wa mapokezi ya Makamu Mwenyekiti wa CCM, Mzee Steven Wasira jana.

Wana CCM hao wameonyesha hasira zao kufuatia kauli ya Mwenyekiti wa chama hicho Tundu Lisu aliyetoa shutuma akieleza hofu ya kushambulia huku akikinyooshea kidole Chama tawala.

"Tundu Lisu madam ameingia katika Ngoma ya kushindana na CCM ni bora akasubiri majukwaani asitafute kiki" alisema mmoja wa Wana CCM hao. Katika mkutano huo CCM imeeleza kujipanga kuhakikisha Mgombea wake Dkt Samia Suluhu Hassan anashinda kwa kishindo ili aendelee kuongoza Dola.

# Dkt Samia ataka umeme wa kujitosheleza nchini

NA MWANDISHI WETU

NIA ya Rais wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan ni kuona nchi inajitoshelaza kwa nishati ya umeme, ambapo dhamira yake ni kuhakikisha vyanzo vyote vilivopo nchini vinafikisha idadi ya Megawati 4,000 mwaka 2025.

Hayo yamewekwa wazi na Naibu waziri Mkuu na waziri wa Nishati Dkt Doto Biteko, alipoeleza mpango wa Tanzania kuimarisha muunganiko wa Afrika kwa kuwa na Nishati safi ya kupikia.

Amesema kuwa, Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kukuza upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani Afrika, jitihada ambazo zimeungwa mkono na mkakati wa kitaifa na kujumuishwa katika Azimio litakalotiwa saini katika mkutano huu, huku akitoa wito wa ahadi na ushirikiano zaidi katika kuboresha upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani mwetu.

Aidha, amesisitiza kuwa ifikapo mwisho wa mwaka 2025, uwezo wa Tanzania kuzalisha umeme utaongezeka hadi megawati 4,000, nishati inayotoka kwenye vyanzo safi na mbadala inavyonufaisha wakazi wa vijijini na mijini, huku miundombinu ya umeme ikifikia vijiji vyote 12,318 nchini.

Alisema Tanzania inaimarisha muunganiko wa Afrika kwa kuwa na miundombinu ya umeme inayounganisha nchi za Kenya, Burundi, Rwanda, na Uganda, huku miundombinu ya kuunganisha Zambia ikiwa inaendelea.

Pia alitaja miongoni mwa mambo mengine yatakayofanyika katika mkutano huo kuwa ni kushirikishana uzoefu; kupata ahadi muhimu za kisiasa; kutumia ushirikiano ili kufungua uwekezaji wa sekta binafsi; kuanzisha ushirikiano wa kufadhili miundombinu ya nishati; na kukubaliana mfumo wa ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kiashiria cha Ufuatiliaji wa Maazimio ili kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye Mkutano huo.

Ametwataka viongozi walioshiriki mkutano huo kutumia fursa hiyo kuhitimisha Maazimio yanayoendana na matarajio ya bara la Afrika ya nishati na kuimarisha ushirikiano unaohitajika katika kuyatekeleza.

â€œNi matarajio yangu kwamba, mamlaka zinazohusika za nishati katika kila nchi ya majaribio zitajitahidi kuhakikisha maazimio ya nishati yanafanikishwa kupitia malengo na mipango ya hatua zinazolenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme, matumizi ya nishati safi ya kupikia, nishati mbadala na mchango wa mtaji wa sekta binafsi katika kufanikisha upatikanaji wa nishatiâ€ , amemalizia Dk Biteko.

Kwa upande wake Rais wa Benki ya Dunia (WB), Ajay Banga amesema kuwa Bara la Afrika linaweza kubadilisha sura ya Afrika kwa kuwa na juhudi za pamoja za kuunganisha rasilimali zilizopo kuhakikisha nishati ya umeme inawafikia wananchi wengi zaidi Afrika ifikapo 2030

Nae Rais wa Benki ya Afrika (AfDB), Dk Akinumwi Adesina ameipongeza nchi ya Tanzania kwa kuwa mfano wa kuigwa kwa kufanya vizuri katika uwekezaji wa miundombinu ya umeme kwa kuwafikishia nishati ya umeme wananchi katika vijijini vyote 12,318.

Mkutano huo umewakutanisha Mawaziri wa Nishati, Viongozi wa Taasisi za Kimataifa za Kifedha, Wataalam na Wadau wa Mashirika ya Kiraia ambao watapata fursa ya kujadili na kukubaliana malengo, vipaumbele vya sera, suluhisho, na ahadi za jinsi ya kutekeleza Mpango wa Mission 300.

# CCM DAR WASEMA MITANO KWA DKT SAMIA IPO TU

NA MWANDISHI WETU

WANA CCM waliohidhuria mapokezi ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Mzee Steven Wasira juzi waliapa kuhakikisha Mgombea wa CCM nafasi ya Urais Dkt Samia Suluhu Hassan, anashinda kwa kishindo na kuongoza tena kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Wamesema kuwa Imani hiyo inatokana na mshikamano na umoja uliopo kati yao, pia kukubaliwa Kwa chama hicho kutokana na kutimiza ahadi zilizomo katika Ilani yao ya uchaguzi.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Stevin Wasira, amesema idadi kubwa ya wanachama waliosajiliwa ndani ya chama hicho inatosha kukifanya CCM kuendelea kushika dola na kubaki madarakani.

Wasira alitoa kauli hiyo leo, Januari 23, 2025, baada ya kupokewa na wanachama wa CCM katika Makao Makuu ya chama hicho, jijini Dodoma. Akizungumza mbele ya mamia ya wanachama waliojitokeza, Wasira alisema, "Kwa mtaji wa wanachama tuliowasajili, CCM ina nguvu ya kuendelea kushika madaraka na kuleta maendeleo endelevu kwa Watanzania."

Akiwa kwenye mkutano huo, Wasira aliwakumbusha wanachama na viongozi kuwa mwaka 2025 ni mwaka muhimu wa uchaguzi wa Rais, Wabunge, na Madiwani, na hivyo aliwataka wanachama waendelee kuwa imara na kushirikiana kuhakikisha chama kinapata ushindi wa kishindo.

"Huu ni mwaka wa uchaguzi, ni lazima tuhakikishe tunadumisha mshikamano, tukitekeleza sera zetu kwa ufanisi, na kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa uadilifu," alisisitiza Wasira.

# Safari za Treni zaongezeka

NA MWANDISHI WETU

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limetangaza kuongeza huduma za treni za mijini kati ya Stesheni ya Kamata na Pugu, jijini Dar es Salaam kwa siku kuanzia jana kutokana na kufungwa kwa baadhi ya barabara za kuingia katikati ya jiji kutokana na mkutano wa nishati wa wakuu wa nchi za Afrika.

Kwa mujibu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano, Fredy Mwanjala imezitaja treni hizo kuwa ni ya Stesheni ya Kamata na Pugu. Mwanjala amesema treni zilizoongezwa ni ya saa 12.00 asubuhi kutoka Stesheni ya Kamata na treni ya saa 12.05 jioni kutoka Stesheni ya Pugu.

"Shirika la Reli Tanzania linapenda kuwatangazia kuwa kutokana na kufungwa kwa barabara za kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam kufuatia mkutano wa nishati wa wakuu wa nchi za Afrika, shirika limeongeza treni mbili za mjini kati ya Stesheni ya Kamata na Pugu, Jijini Dar es Salaam kwa siku ya Januari 27 na 28, 2025" imeeleza taarifa hiyo.

Hata hivyo, Mwanjala alisema pamoja na hatua hiyo ratiba za awali za treni zitabaki kama kawaida.



# Dkt. Samia aridhishwa na maendeleo mji wa Kibaha

NA MWANDISHI WETU

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, ameweka wazi kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia Halmashauri ya Mji wa Kibaha kupandishwa hadhi na kuwa Manispaa.

Mchengerwa ameeleza kuwa taratibu za mwisho zinafanywa, na kutatangazwa rasmi kuwa Manispaa hivi karibuni.

Ameeleza hayo katika mkutano wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoani Pwani uliofanyika Mailmoja, Kibaha, mkutano ulioandaliwa kupongeza na kuunga mkono azimio la mkutano Mkuu maalum wa CCM uliofanyika Dodoma, kumchagua Mwenyekiti CCM Taifa Dkt Samia Suluhu Hassan kugombea kiti cha Urais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Mchengerwa alisema kuwa tangu Rais Samia aingie madarakani, tayari ameunganisha vitongoji kuwa vijiji na vijiji kuwa miji kulingana na vigezo na utaratibu ulio wazi.

"Kwa namna mji wa Kibaha ulivyokuwa, hakuna sababu mji huu usiwe Manispaa. Rais Samia kwa kushirikiana na viongozi wa mkoa, wilaya, na jimbo, ameleta maendeleo makubwa Kibaha na Mkoani Pwani, na hayo ni manufaa ya vizazi vijavyo" alisema Mchengerwa.

Alifafanua zaidi kuwa hakuna anayekataa kwa macho kwamba Rais Samia amefanya kazi inayoonekana na ameacha alama katika sekta zote, huku wananchi wakiwa mashahidi wa maendeleo hayo.

Kwa mujibu wa Mchengerwa, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Rufiji na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Pwani (MNEC), Mkoa huo ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa kura, na tutaakikisha hakuna kura inayopotea wakati wa uchaguzi.

MNEC huyo aliwataka madiwani, wabunge, na wanachama wa CCM kuendelea kukisemea chama kwa kueleza utekelezaji wa ilani na miradi iliyotekelezwa.

Naye Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini, Silvestry Koka, alifurahi na kuishukuru Serikali kwa uamuzi huu baada ya maombi yao ya muda mrefu ya kuhakikisha mji wa Kibaha unakuwa Manispaa.

"Katika mji wetu, yaliyofanyika ni mengi kama maajabu, lakini Rais Samia anafanya maajabu zaidi. Mfano, mwaka 2010 wakati naingia madarakani, lami pekee ilikuwa kuanzia Tamco â€" Hospitali ya Tumbi hadi Pichandege. Leo hii, karibu kila kata ina barabara ya lami na ambazo hazijakamilika zinakwenda kutandazwa lami katika kata zote" alibainisha Koka.

Koka alieleza kuwa kwa sasa Kibaha ina hospitali ya wilaya Lulanzi, vituo vya afya, umeme kila kona, miundombinu ya barabara, na ujio wa barabara sita katika barabara kuu ya Morogoro. Pia, nishati ya umeme, maboresho katika sekta ya elimu, na maji safi vimeendelea kutekelezwa, ambapo imebakia kata ya Pangani ambayo kuna mradi unaendelea, na ukikamilika kero hiyo itakuwa historia.

"Maendeleo haya yote ni matunda ya jitihada zilizofanywa na Serikali, madiwani, jimbo, na usimamizi wa CCM, na ndio sababu ya kupanda hadhi Halmashauri yetu kuwa Manispaa" aliongeza Koka.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani, Mwinshehe Mlao, alitoa tamko la Mkoa wa Pwani kuunga mkono Mkutano Mkuu maalum wa CCM kumchagua Mwenyekiti wa CCM Taifa kugombea nafasi ya Rais kwa tiketi ya CCM katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Pia, walimpongeza Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza kupitia CCM katika uchaguzi huo.

Kadhalika, Mlao amempongeza Rais wa Zanzibar, Hussein Mwinyi, kuwa mgombea wa nafasi ya Rais kupitia CCM Zanzibar.

# Mkurugenzi azindua Kitabu malezi ya watoto

NA HUSNA NASSORO

MWANDISHI wa kitabu cha Elimu na Malezi kwa Watoto Katika Zama za Kidijitali ambaye pi ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro Dkt. Haji Mnasi amezindua kitabu hicho katika kijiji cha Kitangari Sokoni kilichopo wilayani Newala mkoani Mtwara.

Uzinduzi wa kitabu hicho umefanya juzi katika Uwanja wa Mpira Shule ya Msingi Kitangari B.Dkt. Mnasi amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumuamini huku akisema licha ya kuwa na majukumu mengi ya kiserikali ila aliwiwa kuandika kitabu hicho kutokana na kasi kubwa ya ukuaji wa utandawazi ambao umeelezwa kuathiri mila na tamaduni za taifa.

â€œKitabu hicho kinaenda kuwa suluhisho katikati zama hizi za utandawazi na ukuaji wa teknolojiaâ€ , alisema,Dkt. Haji Mnasi.

Hivyo Dkt. Haji Mnasi amewataka wazazi, walezi pamoja na jamii kupata nakala za kitabu hicho ili kuwasaidia watoto katika namna bora ya kujifunza na kupata elimu pamoja na malezi yaliyo bora ili kukuza taifa lenye maadili mema, uchapakazi kama ambavyo maono ya Rais Samia Suluhu yamekuwa yakijikita katika kusisitiza ujenzi wa jamii bora na kizazi salama cha kesho.

# RAIS SAMIA ASUBIRIWA KWA NENO LAKE AFRIKA



NA MWANDISHI WETU

WAKATI Mkutano wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika ujulikanao kama Mission 300, ukiwa umeanza jana, Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa â€˜kuishusha pumziâ€™ Afrika pale atakapounguruma kwenye mkutano huo leo

Rais Dkt. Samia ambaye amejitwisha zigo la kuipigania nishati safi, anatarajiwa kusikilizwa na wengi haswa kina mama wa Afrika, ambao wengi wana matarajio makubwa naye ya kuwasemea juu ya adha wanazopata kutokana na ukosefu wa nishati safi.

Akiwa ameibeba ajenda ya nishati salama mkononi mwake, Rais Dk. Samia amevunja na kuandika rekodi ya aina yake kwa kuwa Rais wa kwanza nchini aliyewahi kupokea idadi kubwa ya wakuu wa nchi 25 kujai kwa pamoja nchini.

Nchi ambao wakuu wake wamethibitisha kushiriki ni Algeria, Comoro, Liberia, Lesotho, Botswana, Kenya, Ghana, Gabon, Sierra Leone, Ethiopia, Sudan, Malawi, Zambia, Somalia, Guine Bisau, Burundi, Mauritania, Kongo Brazzaville, Madagascar, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Libya, Nigeria, Djibouti na Gabon.

Wakati akizungumzia kwa kina mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt.Doto Biteko alisema, utakuwa ni fursa kubwa sana kwa Watanzania.

“Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana ya kuitangaza Tanzania kimataifa, hii imepeleka taasisi za kimataifa, kampuni na wawekezaji kuona Tanzania kuwa ni sehemu sahihi ya kufanya biashara na uwekezaji na mfano halisi ni Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo Afrika kuichagua Tanzania kufanya mkutano huu mkubwa wa kimataifa utakahudhuriwa viongozi kitoka nchi 54 barani Afrika.” Amesema Dkt. Biteko

Ameongeza kuwa, sababu nyingine kubwa ya Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano huo ni mafanikio yaliyofikiwa katika sekta ya nishati ikiwa ni pamoja na kupeleka umeme kwa wananchi suala linaloendanana Ajenda ya mkutano huo ya kuharakisha kupeleka umeme kwa wananchi milioni 300 barani Afrika ifikapo 2030 kati ya watu milioni 685 ambao bado hawana umeme.

“Taifa limepiga hatua kubwa katika Sekta ya Nishati, tunamshukuru Rais kwa msukumo mkubwa anaotoa katika Sekta ya Nishati, taifa lina umeme wa kutosha na wa ziada, uzalishaji sasa umepanda kutoka megawati 1470 hadi megawati takriban 3,077.”

Amesema upatikanaji wa umeme barani Afrika kwa sehemu kubwa uko chini ya asilimia 50 lakini Tanzania imepiga hatua kubwana ipo kwenye asilimia zaidi ya 78.

Akiongeza kuhusu mafanikio ya Sekta ya Nishati, Dkt. Biteko amesema vijiji vyote 12,318 Tanzania sasa vimesambaziwa umeme na tathmini iliyofanywa na Benki ya Dunia barani Afrika mwaka jana imeonesha kuwa Tanzania iliongoza kwa kusambazia wananchi umeme vijijini .

Dkt. Biteko ameeleza kuwa, baada ya umeme kufika kwenye vijiji vyote sasa kasi inaelekea kwenye vitongoji ambapo katika vitongoji 64,000 nchini, vitongoji takriban 36,000 vimepelekewa umeme.

Ametaja faida za mkutano wa M300 kwa Tanzania kuwa ni pamoja na kuongeza fursa za kupata fedha za kuendelea miradi mbalimbali, kuongeza fursa za uwekezaji, kupata uzoefu kutoka kwa waliofanikiwa zaidi kwenye sekta ya nishati na kuongeza heshima ya nchi kimataifa.

Ameongeza kuwa faida nyingine ni kuharakisha upatikanaji umeme nchini ambapo kiasi cha wananchi watakaounganishiwa umeme kupitia M300 ni milioni 8.3 ifikapo 2030 na hivyo kuifanya Tanzania kuunganisha wateja milioni 13.5 kufikia 2030 Kutoka milioni 5.2 ya sasa.

Wakati huohuo, nchiza Afrika zimeelezwa kupiga hatua katika suala zima la upatikanaji nishati ya umeme toka nyingi kati ya hizo zipte uhuru miaka ya 1960.

Akisema hilo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema baada ya kupata uhuru, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao.

Dk. Biteko alisema hayo jana kwenye Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika ‘Mission 300’ unaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es salaam

â€œInasikitisha kwamba idadi ya Waafrika ambao hawana umeme inakadiriwa kuwa milioni 571.kutokana na hali hii, Mkutano huu uliitishwa, ukiwa na lengo kubwa lakini linaloweza kufikiwa la kuongeza upatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

Kama ilivyobainishwa katika Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), leo Dar es Salaam inayo heshima ya kuwa mwenyeji wa wajumbe kutoka Afrika na kwingineko, wakihudhuria Mkutano huu muhimu unaolenga kuimarisha azma ya Afrika ya kuipatia bara hili nishati.

“Baada ya kupata Uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao. Tanzania ilikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 21 pekee wakati wa Uhuru, kwa sasa nchi ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,160.”

SOMA ZAIDI UK 8&9

# MKUTANO WA M-300 UNATAZAMWA



LEO na kesho mataifa yote ya Afrika yataelekeza macho yake ndani ya Tanzania wakati mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu nishati ukiwa umebeba ajenda kuu ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa wakazi wote wa bara hili.

Mkutano huo uliopewa jina la Mission 300 (M300) unaongozwa na kaulimbiu inayosema: 'Kuharakisha upatikanaji wa Nishati Afrika', ukiwa na malengo ya kujadili dhana nzima ya upatikanaji wa umeme kwa wote hususan katika nyakati ambazo viongozi wa Afrika wanasisitiza matumizi ya nishati safi na salama.

Tanzania itanufaika na mkutano huo hasa ikizingatiwa kuwa wakuu wa mataifa hayo wataidhinisha Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika, ambao wakuu hao wanakubaliana kufanya mageuzi yatakayosaidia kufikia lengo la upatikanaji wa nishati kwa wote kwa njia za kuaminika, nafuu na endelevu.

Takwimu za nishati kwa Afrika zinaonesha kuwa hadi mwaka 2022 asilimia 83 ya watu milioni 685 walikuwa hawajafikiwa na nishati hiyo. Kwa msingi huo, mkutano huo unadhamiria kuhimiza kuchukuliwa kwa hatua mbalimbali, ikiwemo kuingia makubaliano ili umeme uwafikie watu milioni 300 ifikapo mwaka 2030.

Katika mkutano huo wenye azma ya kuwafikia watu hao milioni 300, nchi 14 zitasaini Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika Awamu ya Kwanza.

Nchi hizo ni Tanzania, Malawi, Chad, Nigeria, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Niger, Liberia, Msumbiji, Madagascar, Zambia, Mali, Ivory Coast na Mauritania.

Diplomasia ya kiuchumi ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na nia yake thabiti ya kuibeba ajenda ya nishati safi, ndiyo imefanikisha ujio mkubwa wa viongozi wakuu wan chi za Afrika, ambao wanakutana jijini Dar es Salaam ili kujadili nishati safi na salama.

Akiwa ameibeba ajenda ya nishati salama mkononi mwake, Rais Dk. Samia anatarajiwa kuvunja na kuandika rekodi ya aina yakwe kwa kuwa Rais wa kwanza nchini aliyewahi kupokea idadi kubwa ya wakuu wa nchi 25 kujai kwa pamoja nchini.

Kwetu tunaamini mkutano huo utatoka na majibu ya kina juu ya matatizo ya upatikanaji wa nishati hiyo kwa wakazi wa bara hili na tunawaombea wote heri kubwa, wanapokwenda kujadili na kutatua tatizo la nishati ya umeme barani Afrika.

# Mkutano wa Nishati Afrika, Kichocheo Utekelezaji Sera ya Taifa ya Nishati

Na Jacquiline Mrisho - MAELEZO



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa, Tanzania inachukulia mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika - Misheni 300 kama kichocheo cha utekelezaji wa Sera yake ya Taifa ya Nishati inayolenga kuendeleza nishati endelevu, uhifadhi na ufanisi.

Ameyasema hayo leo Januari 27, 2025 wakati akifungua Mkutano huo unaofanyika jijini Dar es Salaam kwa siku mbili kuanzia leo Januari 27 hadi 28, 2025 ambapo majadiliano ya leo yamehusisha ngazi ya Mawaziri na Wadau wa masuala ya nishati na fedha na kesho majadiliano yatahusisha ngazi ya viongozi wakuu wa nchi za Afrika.

Mhe. Dkt. Biteko ameeleza kuwa, pamoja na maendeleo ya nishati tunayojivunia, bado nchi inahitaji uwekezaji zaidi katika sekta ya nishati kwani matarajio yake ni kukuza shughuli za kiuchumi hususan katika sekta za viwanda, madini na huduma za ukarimu jambo ambalo linahitaji uwekezaji wa kimkakati zaidi katika sekta ya nishati.

"Sera hiyo pia inalenga kuongeza upatikanaji wa huduma za kisasa za nishati na kuongeza mchango wa nishati mbadala katika mchanganyiko wa uzalishaji ili kuimarisha upatikanaji, uhakika na usalama wa nishati", amesema Dkt. Biteko.

Ameongeza kuwa, Rais wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kukuza upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani Afrika, jitihada ambazo zimeungwa mkono na mkakati wa kitaifa na kujumuishwa katika Azimio litakalotiwa saini katika mkutano huu, huku akitoa wito wa ahadi na ushirikiano zaidi katika kuboresha upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani mwetu.

Aidha, amesisitiza kuwa ifikapo mwisho wa mwaka 2025, uwezo wa Tanzania kuzalisha umeme utaongezeka hadi megawati 4,000, nishati inayotoka kwenye vyanzo safi na mbadala inavyonufaisha wakazi wa vijijini na mijini, huku miundombinu ya umeme ikifikia vijiji vyote 12,318 nchini.

Pia, Tanzania inaimarisha muunganiko wa Afrika kwa kuwa na miundombinu ya umeme inayounganisha nchi za Kenya, Burundi, Rwanda, na Uganda, huku miundombinu ya kuunganisha Zambia ikiwa inaendelea.

Ametaja miongoni mwa mambo mengine yatakayofanyika katika mkutano huo kuwa ni kushirikishana uzoefu; kupata ahadi muhimu za kisiasa; kutumia ushirikiano ili kufungua uwekezaji wa sekta binafsi; kuanzisha ushirikiano wa kufadhili miundombinu ya nishati; na kukubaliana mfumo wa ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kiashiria cha Ufuatiliaji wa Maazimio ili kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye Mkutano huo.

Ametoa rai kwa viongozi walioshiriki mkutano huo kutumia fursa hiyo kuhitimisha Maazimio yanayoendana na matarajio ya bara la Afrika ya nishati na kuimarisha ushirikiano unaohitajika katika kuyatekeleza.

"Ni matarajio yangu kwamba, mamlaka zinazohusika za nishati katika kila nchi ya majaribio zitajitahidi kuhakikisha maazimio ya nishati yanafanikishwa kupitia malengo na mipango ya hatua zinazolenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme, matumizi ya nishati safi ya kupikia, nishati mbadala na mchango wa mtaji wa sekta binafsi katika kufanikisha upatikanaji wa nishati", amemalizia Dkt. Biteko.

Kwa upande wake Rais wa Benki ya Dunia (WB), Bw. Ajay Banga amesema kuwa bara la Afrika linaweza kubadilisha sura ya Afrika kwa kuwa na juhudi za pamoja za kuunganisha rasilimali zilizopo kuhakikisha nishati ya umeme inawafikia wananchi wengi zaidi Afrika ifikapo 2030

Nae Rais wa Benki ya Afrika (AfDB), Dkt. Akinumwi Adesina ameipongeza nchi ya Tanzania kwa kuwa mfano wa kuigwa kwa kufanya vizuri katika uwekezaji wa miundombinu ya umeme kwa kuwafikishia nishati ya umeme wananchi katika vijijini vyote 12,318.

Mkutano huo umewakutanisha Mawaziri wa Nishati, Viongozi wa Taasisi za Kimataifa za Kifedha, Wataalam na Wadau wa Mashirika ya Kiraia ambao watapata fursa ya kujadili na kukubaliana malengo, vipaumbele vya sera, suluhisho, na ahadi za jinsi ya kutekeleza Mpango wa Mission 300.

# CCM INA SERA KIMBILIO KWA WANYONGE

NA MWANFDISHI WETU

CHAMA cha Mapinduzi CCM, kinaendelea kukubalika zaidi kutokana na kufanikiwa kutekeleza aslimia kubwa ya Ilani ya uchaguzi na kuleta maendeleo, yanayoonekana machoni mwa Watanzania.

Uimara wa chama hicho unazidi kuonekana kadri siku zinavyoizidi kwenda kuelekea uUhaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, ambapo chama hicho tawala, kimemsimamisha mwenyekiti wake na Rais wa sasa Dkt Samia Suluhu Hassan ambaye anaonyesha kuwa na mvuto wa hali ya juu.

Ukiacha kukubalika kwa chama hicho kikongwe, hivi karibuni CCM ilifanya uchaguzi wake kuwaletea wanachama wake Makamu Mwenyekiti Bara anayekitambua na kuwa mtaji mkubwa, kuelekea uchaguzi huo.

CCM ilimchangua Makamu mwenyekiti Mzee Steven Wassira ambaye licha ya kukubalika na kufahamu chama hicho lakini amekuwa mzoefu hasa katika masuala ya uchaguzi kutokana na kuhudumu katika nafasi mbali mbali za chama na serikali tangu nenzi ya chama cha Tanu.

Kutokana na uimara wa CCM ni wazi kuwa Mwanasiasa Tundu Lissu anayetajwa na Chamdema kama silaha yake katika uchaguzi Mkuu, bado anaonekana kutofua dafu kutokana na ushawishi mdogo aliokuwa na vilevile ugeni katika nafasi ya Uenyekiti, huku pia akionyesha dhaoifu katika kuchukua uamuzi.

Kundi kubwa la wanachama na wapenzi wa Chadema waliokuwa wakitamani kumuona aliyekuwa Mwenyekiti wake wa miaka mingi Freeman Mbowe akirejea katika kiti chake hicho ni kikwazo pia kwa Tundu Lisu ambaye anaweza kusababisha chama kusambaratiba na wanachama wake kumiminika na kupokelewa na kuwa na amani mioyoni mwao ni ndani ya CCM.

Ndiuyo maana hivi karibuni iliweka wazi kuwa kuna kasi kubwa ya viongozi na wanachama wa vyama vya upinzani kukimbilia chama hicho ni kutokana na utekelezaji mzuri wa ajenda zenye mvuto kwa vyama vya upinzani.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla alisema hayo hivi karibuni Dodoma katika mada ya Kuelekea Mkutano Mkuu wa CCM, ambapo Makalla alisema kutokana na uongozi bora wa Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi, CCM imevuna wanachama wengi vijana hali inayofanya kuwa na wanachama wanaofikia zaidi ya milioni 10.

Alisema chama kimefanikiwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kwa asilimia kubwa kutokana na uharaka wa Rais Samia kutoa fedha za miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema kutokana na ufanisi katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, wananchi waliamua kukipa ridhaa chama katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024.

"Ushindi wa kishindo wa CCM katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024, ni ishara nzuri kuwa wananchi wameridhishwa na sera, itikadi na utekelezaji wa ilani ya chama" aliongeza Makala.

Kuhusu Mapinduzi ya Zanzibar kufikisha miaka 61, Makalla alisema Zanzibar imeandika historia yake yenyewe na ni kitendo cha kizalendo na cha kujivunia.

Alifafanua Mapinduzi ya Zanzibar yalikuwa lazima yafanyike ili kuondoa unyonge, manyanyaso, dhuluma na ubaguzi kutoka kwa wakoloni ili kuboresha huduma za kijamii kama maji, elimu, afya na miundombinu ya barabara.

Mkutano Mkuu wa CCM unatarajiwa kufanyika Januari 18 na 19, mwaka huu mkoani Dodoma na miongoni mwa mambo yanayotarajiwa kufanyika ni kujaza nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara baada ya Abdulrahman Kinana kuomba kupumzika.

Kabla ya kushika nafasi hiyo, Kinana alishika nyadhifa mbalimbali ndani ya chama na serikali ikiwamo ya Katibu Mkuu wa CCM.

CCM inakila uhakika wa kuendelea kuzoa wanachama kutoka vyama vya upinzani kutokana na taharki za mvurugano zinavyoendelea kuvitafuna vyama hivyo hali itakayosababisha wanachama wapenda amani kukaa mbali nanavyo na kutafuta sulkuhusu ndani ya CCM.

Tayari joto la mkutano huo likizidi kuonekana Jijini Dodoma ambako wajumbe wengi wamshawasili tayari kwa tukio hilo kubwa na la Kihistoria linalitazamiwa kuvuta hisia za wafuatiliaji wengi wa masuala ya kisiasa ndani na nje yta nchi.



NA MWANDISHI MAALUM

# Wapinzani wanavyopiga hesabu kuivaa

SAFU mpya ya uongozi wa CCM iliyokamilika hivi karibuni imekuwa mwimba mchungu, kwa wanasiasa wa vyama vya upinzani, ambayo ndiyo kwanza wanajipanga huku siku za kufanyika uchaguzi mkuu zikienda mbio.

Uchunguzi wa gazeti hili umebaini kuwepo kwa mikakati ya haraka inayofanywa ndani ya vyama hivyo ili kupanga safu za uongozi na hasa wale watakaopendekezwa kusimama kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika mwezi Oktoba.

Kwa mfano Chadema ndiyo kwanza hivi sasa inahaha kupokea majina ya wanachama na kuyafanyia upembuzi ili yaweze kuwekwa katika nafasi za kugombea Ubunge na udiwani pindi uchaguzi mkuu utakapowadia.

Katika kuhakikisha upembuzi huo unafanyika kwa uhakika chama kimekuwa na kazi kubwa ya kushirikisha Wanachadema ambao wengi hawana uzoefu na uongozi ili kupata majina sahihi.

Hiyo inatokana na ugeni wa Mwenyekiti aliyeshinda kiti hicho hivi karibuni Tundu Lissu ambaye licha ya kuagiza umakini mkubwa unahitajika kupata wawakilishi wa chama lakini pia amekuwa akihofia kuingiza mamluki watakaoweza kumsaliti hapo baadaye.

Tundu Lissu aliingia madarakani tarehe Januari 21,2025 na kuwa na kukumbukwa ambayo Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kilizaliwa upya kikiwa na sura mpya ya uongozi, huku mwanasiasa machachari Tundu Lissu akikabidhiwa jukumu la kuwa nahodha wa kulifikisha salama jahazi lao.

Lissu anakuja katika kipindi ambacho chama kinaingia katika uchaguzi Mkuu wa rais wabunge na Madiwani hapo Mwezi Oktoba, huku yeye akitakiwa kusimamia safu yake ya kuongozi kukiingiza chama kwenye vuguvugu hilo huku mbele yake kukiwa na ukuta mgumu uliojengwa imara wa Chama Cha Mapinduzi CCM.

Chadema kinachoogelea katika historia ya vyama vyenye nguvu nchini kimeongeza historoa kubwa ya kuhitimisha safari ya Mwenyekiti Freeman Mbowe kuwa mwenyekiti kwa kiuhudumu kwene nafasi hiyo kwa miaka 21.

Itakumbukwa kwamba 2019/2020 CCM ilipita bila kupingwa na kupata Ushindi nchi nzima katika Uchaguzi na hakuna hatua za makusudi zilichukuliwa na Chadema kukabiliana na hali hiyo kuelekea uchaguzi wa 2024.

Yaliyofanyika 2019/2020 yamejirudia tena 2024 ambapo CCM imeshinda tena kwa asilimia 100.

Kwa vyovyote suala hilo litatokea tena Uchaguzi mkuu 2025 kwani sioni Chadema iliyojipanga kushindana katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Haijalishi CCM inashindaje (mbinu) inaitwa imeshinda kwa sababu mamlaka za Usimamizi wa uchaguzi hutangaza na hakuna hatua za kisheria kwa mujibu wa kanuni na Sheria za uchaguzi Chadema inachukua, ndiyo maana kilichofanyika 2019 ndicho kimetokea 2024.

Dhamira ya CCM ni kuua Chadema, na Mbowe amekubali Chadema ife ifikapo 21.01.2025, ambapo Freeman Mbowe anapambania matamanio ya CCM kumfanya yeye kuwa Mwenyekiti. Iwapo atashinda, ushindi wake, utakifanya Chadema kuwa vuguvugu au baridi kabisa.

Bali ushindi wa Tundu Lissu kuwa Mwenyekiti kutaifanya Chadema kuwa ya moto kupita kiasi, atawashughulisha CCM na serikali yake katika masuala yanayohusu haki za kisiasa, Kijamii kiuchumi sambamba na raslimali za nchi.

Siku Chadema itakapokufa ndipo CCM itakapokosa mshindani halisi na kwa mantiki hiyo badala ya kukinyooshea kidole Chadema, badala ya wanaonewa CCM kukimbilia Chadema watatafuta majawabu magumu ndani ya CCM, mtakua na mnyukano isiyoisha nchi itavimba.

Wananchi wakiendelea kukasirika dhidi ya dhuluma za haki za ki uchaguzi kama ilivyotokea mwaka 2019, 2020, 2024 sehemu ya kupumulia makasiriko yao na kulalamikia ilikuwa ni Chadema.

Kifo cha Chadema katika mikono ya Mbowe, maana yake nchi itavimba wataipumulia CCM na serikali yake, nchi itakua ngumu na misuguano isiyokwisha.

Kwa hiyo CCM kushabikia kifo cha Chadema ni maandalizi ya CCM yenyewe kufa. Jambo muhimu ni kuwaacha watu na uamuzi wa kiitikadi badala ya kuwalazimisha wakate tamaa na Chadema.

Hasira zao na makasiriko yao watamalizia CCM, kitakua ni restless party.

CCM isiposhindana itakuwa dhaifu zaidi ya ilipo leo. Ukweli ni kwamba kadri nchi inavyozidi kuwa na vyama vya upinzani imara ndivyo vinafanya chama tawala kuwa imara na kuongeza uwajibikaji kwa wananchi.

Uwajibikaji huo unawaridishia mavuno ya kura kwenye chaguzi zijazo ni hesabu rahisi tu!.

Leo Watanzania wakikosa matumaini na Chadema kinachofuata ni kukosa matumain na chama kilichopo madarakani, hivyo wananchi hulazimika kuchukua hatua mikononi na kuyapata matumaini wayatakayo kwa nguvu.

Kama ingekuwa ni amri yangu, ningesisitiza viongozi waandamizi wa CCM na CCM yenyewe ama serikali kwa namna moja ama nyingine isijihusishe kukiua Chadema kama walivyofanya kwa CUF, NCCR MAGEUZI na TLP, wakiache kama ambavyo CCM huachwa ifanye Uchaguzi wake bila kuingiliwa.

Ningesisitiza pia kwamba Chadema kifanye chaguzi zake bila kuruhusu kuingiliwa au kuingiza maslahi kutoka CCM ama taasisi yoyote ya kiserikali.



Mawazo kwa kuwa na Chama kimoja huku vingine vikibaki kama Matawi ya CCM, ni ya hatari.

Ikitokea hali hiyo, hapo ndipo utabiri wa Mwalimu Nyerere kwamba: CCM itaondolewa na wana CCM/watu waliotoka CCM wenyewe ndipo utakapotimia. Msuguano na vita ndani ya CCM itakuwa kubwa kuliko kawaida.

Muda ni Mwalimu mzuri, kifo cha Chadema hakiifanyi CCM kuwa Imara isipokuwa ni kujichimbia kaburi ambalo mtazikwa wenyewe.

Turejee kwenye sababu za msingi za kuanzishwa kwa vyama vya nchini Tanzania 1992.CHADEMA imara itajenga mazingira ya CCM imara zaidi.

# Tanzania inavyovutia kwa maendeleo

NA MWANDISHI WETU



MAENDELEO yanayofanyika ikiwemo ujenzi wa Miundombinu ya Barabara, Reli ya kisasa, Hospitali, Zahanati na maboresho katika sekta ya elimu ni miungoni mwa mambo yanayowavutia hata wananchi wanaoshi katika nchi jirani na Tanzania.

Wananchi wa Kenya wanapotembelea Tanzania mara nyingi wamekuwa wakiweka wazi juu ya kuvutiwa kwao na maendeleo wanayokutana nayo katika miji ya Tanzania, ambayo miaka ya nyuma walikuwa wakiiona katika nchi yao.

Kwa sasa kinachovutia Wakenya wengi ni uwepo wa Treni ya kisasa inayofanya safari zake katika miji ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma ambayo kwao wanafananisha na ile inayotumika katika nchi zilizoendelea hususan katika Bara la Ulaya na Marekani na nchi zilizoendelea.

Baadhi ya Wakenya waliozungumza na gazeti hili, wanaweka wazi jisni gani maendeleo ya Tanzania wanavyoyaona yakilipita taifa lao, huku wakijiuliza nini kilichofanyika katika nchi hii jirani yao, ambacho kwao hakiwezei.

Ukiacha Wakenya hata mjirani wengine kutoka nchini Malawi nao wanayasifia maendeleo ya Tanzania, kwamba yanakuwa ni mfano wa kuigwa katika nchi za ukanda wa Maziwa Makuu, hasa kukua haraka kiuchumi na maendeleo mengine yanayoonekana wazi.

Wanakumbusha kwamba mnamo miaka ya 1990 Majiji ya Malawi kama vile Blantire, Lilongwe na hata Mzuzu yalikuwa ndiyo safi zaidi miungoni mwa nchi za jirani ikiwemo Tanzania.

Miji hiyo ndiyo iliyoanzisha mpango wa kusafishwa usiku kabla ya Dar es salaanm na Nairobi hayajaanza kupata huduma hiyo, lakini matokeo yake hivi sasa wameachwa mbali kimaendeleo.

Katika mika hiyo Barabara ya Tanzania inayounganisha nchi ya Malawi ilikuwa hajakamilika kwa kiwango cha Lami, hivyo wasafiri wanaotoka nchini walikuwa wakikutana na Barabara za Lami wanapoingia nchini Malawoi hususan katika miji ya mwanzoni kama Kalonga, Lumph, Ekwendeni na Mzuzu kisha kuelekea katika Mji Mkuu wa Lilongwe.

Hata hivyo miji hiyo kwa sasa inakabiliwa na uchakavu wa miundombinu huku Tanzania ikizidi kujenga barabara katika mikoa na wilaya ambazo awali zilikuwa zimejifunga kutoka eneo moja kwenda jingine.

Miradi ya kimkakati ya ujenzi ilianza kushika kasi tangu utawala wa Awamu ya Tano chini ya Rais Dkt hayati John Pombe Magufuli ambapo sasa ndiyo kasi imeongezeka katika utawala wa awamu ya Sita chini ya Dkt Samia Suluhu Hassan.

Kufuatia maendeleo hayo Tanzania inaelekea pazuri na pengine kwa miaka michache ijayo, itakuwa ndiyo nchi kimbilio kwa wananchi mbalimbali kutoka mataifa mengine kama ilivyokuwa Afrika Kusini, nchi inayopokea wageni kila uchao kutokana na kufunguka kwa fursa za kibiashara na maisha.

Hii inatokana na mikakati ya Serikali Awamu ya sita kupitia Ilan ya Chama tawala CCM, ambayo imekuwa ikiratibu maendeleo na kuifanya nchi kuonekana ikipiga maendeleo ya kasi.

Dkt Samia ambaye amekuwa akisimamia kwa makini masuala ya maendeleo, amekuwa mkali kwa wasaidizi wake akiwataka wasifanye ajizi inapobidi kusimamia kazi za kuwatumia Watanzania, ndiyo maana amekuwa mkali na asiyekuwa na subira pale anapogundua uzembe unafanyika sehemu yoyote il anafanya mabadiliko ya haraka.

# TNGP yafanya uchambuzi

NA MWANDISHI WETU

Taasisi isiyo ya Kiserikali ya TGNP Mtandao kwa kushirikiana na Vituo vya Taarifa na Maarifa halmashauri ya Wilaya ya Mbeya vimefanya uchambuzi wa bajeti yenye mrengo wa Kijinsia katika ukumbi wa halmashauri mgeni rasmi akiwa ni Kaimu Mkurugenzi Aliko

Katika hotuba yake Mbuba amesema halmashauri imekuwa ikishirikiana vema na TGNP mara zote walizoshauri halmashauri imekuwa ikichukua hatua mbalmbali hasa kutenga bajeti katika masuala ya afya,elimu,maji na uwezeshaji kiuchumi.Mbuba.

Rose Mwalongo mshauri kutoka TGNP amesema mrejesho umekuwa mzuri hususani katika sekta za afya,maji na elimu ambazo zimelenga mrengo wa kijinsia sanjari na msisitizo wa ushirikishwaji kwa wanaume.

Naye Mhandisi Evetha Nzogela kutoka RUWASA Wilaya ya Mbeya amesema wao katika sekta ya maji wamezingatia mrengo wa kijinsia ili kuyafikia malengo ya serikali hususani ongezeko la upatikanaji wa maji vijijini kwa asilimia 85 ifikikapo mwaka 2025.

RUWASA imekuwa na mpango endelevu hasa kwenye vijiji kwa kujenga vioski vya maji karibu sanjari na kuwahimiza watu kuingiza maji majumbani ili kuondoa migogoro ya ndoa iliyokuwa ikitokea kutokana na wanawake kutafuta huduma ya maji mbali na makazi yao.

Aidha Zawadi Merere ni Mwakilishi wa Kikundi cha Taarifa na Maarifa kutoka Kata ya Tembela ameishukuru TGNP kwa kuwaongezea ujuzi wa kuyapambanua mambo ikiwemo uchambuzi wa bajeti na kujiamini ambapo kwa sasa huduma za afya zimezidi kuimarika katika vijiji mbalimbali katika ujenzi wa zahanati na vituo vya afya zoezi lililosaidia kupunguza vifo kwa mama na mtoto.

Kaimu mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbeya Dkt Mary Mwakyembe amesema changamoto mbalimbali zimetatuliwa zikiwemo za upatikanaji wa dawa pia kadi za kliniki kwani kwa sasa hakuna tena uhaba wa kadi hizo ambapo zahanati zinaruhusiwa kuagiza bohari ya dawa(MSD).

Hata hivyo changamoto ya upungufu wa watumishi sekta ya afya limepungua kwani kila mwaka wamekuwa wakipokea watumishi wapya kupitia serikali na Wizara ya Afya.

TGNP imezidi kuvijengea uwezo vikundi mbalimbali vya taarifa na maarifa mbali kupinga ukatili wa kijinsia imewajengea uwezo wanawake katika kugombea uongozi pamoja na uanzishaji wa miradi ya kiuchumi.



Tanzania BORA



# MKUTANO M300 KUING'ARISHA ZAIDI AFRIKA

NA MWANDISHI WETU




NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema baada ya kupata uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao.

Dk. Biteko amesema hayo kwenye Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika â€˜Mission 300â€™ unaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es salaam

Naibu Waziri Mkuu amesema lengo kuu la mkutano huo kuitishwa ni kufikia lengo la kuongeza upatatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

Inasikitisha kwamba idadi ya Waafrika ambao hawana umeme inakadiriwa kuwa milioni 571.kutokana na hali hii, Mkutano huu uliitishwa, ukiwa na lengo kubwa lakini linaloweza kufikiwa la kuongeza upatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

Kama ilivyobainishwa katika Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), leo Dar es Salaam inayo heshima ya kuwa mwenyeji wa wajumbe kutoka Afrika na kwingineko, wakihudhuria Mkutano huu muhimu unaolenga kuimarisha azma ya Afrika ya kuipatia bara hili nishati.

Baada ya kupata Uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao. Tanzania ilikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 21 pekee wakati wa Uhuru, kwa sasa nchi ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,160.

Pamoja na mafanikio makubwa ya kuzalisha umeme barani Afrika, takriban Waafrika milioni 571 bado hawana huduma ya umeme. Mkutano huu umeitishwa rasmi kwa lengo la kujadili namna ya kuongeza upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Natoa shukrani za dhati kwa waandaaji wenza wa Mkutano huu ikiwemo: Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika; Rockefeller Foundation; Sustainable Energy for All (SEforALL), na The Global Energy Alliance for People and Planet (GEAPP) kwa ushirikiano uliowezesha kufanyika kwa Mkutano huu.

Uwepo wenu, mawazo na utaalamu wenu ndiyo vitakavyofanikisha Mkutano huu. Natarajia majadiliano yenye tija na tushirikiane katika kuunda mustakabali wa nishati barani Afrika.

Natarajia mkutano huu utakuwa ni hatua muhimu katika kufanikisha lengo letu la upatikanaji wa umeme kwa wote.

â€œKatika mkutano huu, Mawaziri wa Nishati, Viongozi wa Taasisi za Kimataifa za Kifedha, Wataalam na Wadau wa Mashirika ya Kiraia, watapata fursa ya kujadili na kukubaliana malengo, vipaumbele vya sera, suluhisho, na ahadi za jinsi ya kutekeleza Mpango wa Mission 300.

Maazimio ya Nishati ya Kitaifa yaliyotayarishwa na nchi 14 zitakazokuwa za majaribio yatatoa mfumo wa utekelezaji wa hatua zilizoratibiwa ili kufungua uwekezaji zaidi kutoka kwa serikali, wabia wa maendeleo, mashirika ya misaada na sekta binafsi katika kufanikisha malengo ya upatikanaji wa nishati.

Kupitia uhamasishaji wa rasilimali na utaalamu katika kuharakisha juhudi za kupeleka umeme barani Afrika, Mission 300 itaonyesha dhamira yetu ya pamoja katika kufanikisha upatikanaji wa nishati safi kwa wote, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na kuboresha maisha ya watu.

Tanzania inachukulia mkutano huu kama kichocheo cha utekelezaji wa Sera yake ya Taifa ya Nishati inayolenga kuendeleza nishati endelevu, uhifadhi na ufanisi. Sera hiyo pia inalenga kuongeza upatikanaji wa huduma za kisasa za nishati na kuongeza mchango wa nishati mbadala katika mchanganyiko wa uzalishaji ili kuimarisha upatikanaji, uhakika na usalama wa nishati.

Ifikapo mwisho wa mwaka 2025, uwezo wa Tanzania kuzalisha umeme utaongezeka hadi megawati 4,000. Nishati yetu inatoka kwenye vyanzo safi na mbadala vinavyonufaisha wakazi wa vijijini na mijini, huku miundombinu ya umeme ikifikia vijiji vyote 12,318 nchini.

Vile vile, Tanzania inamarisha muunganiko wa Afrika kwani ina miundombinu ya umeme inayounganisha nchi za Kenya, Burundi, Rwanda, na Uganda, huku miundombinu ya kuunganisha Zambia ikiwa inaendelea.

Pamoja na maendeleo ya nishati tunayojivunia, bado nchi inahitaji uwekezaji zaidi katika sekta ya nishati. Tuna matarajio ya kukuza shughuli za kiuchumi hususan katika sekta za viwanda, madini, na huduma za ukarimu jambo ambalo linahitaji uwekezaji wa kimkakati zaidi katika sekta ya nishati.

Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kukuza upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani Afrika. Jitihada hizi zimeungwa mkono na mkakati wa kitaifa na yamejumuishwa katika Azimio litakalotiwa saini, huku tukitoa wito wa ahadi na ushirikiano zaidi katika kuboresha upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani mwetu.

Miongoni mwa mambo mengine yatakayofanyika katika mkutano huu, tutashirikiana uzoefu; kupata ahadi muhimu za kisiasa; kutumia ushirikiano ili kufungua uwekezaji wa sekta binafsi; kuanzisha ushirikiano wa kufadhili miundombinu ya nishati; na kukubaliana mfumo wa ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kiashiria cha Ufuatiliaji wa Maazimio ili kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye Mkutano huu.

Ni matarajio yangu kwamba, mamlaka zinazohusika za nishati katika kila nchi ya majaribio zitajitahidi kuhakikisha maazimio ya nishati yanafanikishwa kupitia malengo na mipango ya hatua zinazolenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme, matumizi ya nishati safi ya kupikia, nishati mbadala na mchango wa mtaji wa sekta binafsi katika kufanikisha upatikanaji wa nishati.

Sasa ni wakati wa kufungua uwezo wa nishati wa bara la Afrika na kukabiliana na pengo la nishati. Tuitumie fursa ya Mkutano huu kuhitimisha Maazimio yanayoendana na matarajio yetu ya nishati na kuimarisha ushirikiano unaohitajika kuyatekeleza.

Naye Rais wa Benki ya Dunia (WB), Ajay Banga katika mkutano huo, aliyasema haya;

"Tunaweza kubadilisha sura ya Afrika kwa kuwa na juhudi za pamoja za kuunganisha rasilimali zilizopo kuhakikisha nishati ya umeme inawafikia wananchi wengi zaidi Afrika ifikapo 2030."

Rais wa Benki ya Maendele ya Afrika (AfDB), Dk Akinumwi Adesina alisema: "Tanzania imekua mfano wa kuigwa kwa kufanya vizuri katika uwekezaji wa miundombinu ya umeme kwa kuwafikishia nishati ya umeme wananchi katika vijijini vyote 12,318."

Nawahakikishia kuwa lengo la kuwafikishia umeme watu milioni 300 Afrika linakwenda kufanikiwa, tunahitaji uwazi na uwajibikaji katika kufikisha lengo hili.

"Mkutano huu una lengo la kuifungua Afrika kwenye eneo la nishati ya umeme, kuhakikisha wananchi katika za Afrika wanaunganishwa na umeme."

# Uzalishaji Umeme wa Upepo kwa kutumia Treni



Treni inapokuwa kwenye mwendo wa kasi, husababisha mkondo wa upepo wenye nguvu ambao unaweza kutumika kuzungusha mitambo midogo ya upepo.

**Namna ya Kufanikisha Hili**

Turbine Kando ya Reli Katika maeneo ya wazi, mitambo ya upepo inaweza kuwekwa kando ya reli ili kunufaika na upepo wa asili pamoja na ule unaozalishwa na mwendo wa treni.

**Faida**

Upepo unaosababishwa na mwendo wa treni ni wa kudumu, hasa katika maeneo yenye safari za mara kwa mara.

Inaongeza matumizi ya reli kwa kazi zaidi ya usafiri pekee.

**Changamoto**

Kuweka vifaa vya kuzalisha umeme bila kuathiri mwendo wa treni au kuongeza uzito mkubwa.

**2. Kuzalisha Umeme wa Jua kwa kutumia Treni**

Paneli za sola zinaweza kufungwa juu ya mabehewa ya treni au kwenye maeneo ya karibu na reli ili kuvuna nishati ya jua moja kwa moja.

**Namna ya Kufanikisha Hili**

Paneli Juu ya Mabehewa: Paa za treni zinaweza kufunikwa na paneli za sola zinazoweza kuzalisha umeme kwa ajili ya mifumo ya ndani ya treni kama taa, hewa ya baridi, au kuchaji betri.

Mashamba ya Sola Kando ya Reli: Katika maeneo ya wazi karibu na reli, mashamba makubwa ya sola yanaweza kujengwa. Nishati inayozalishwa inaweza kuhifadhiwa au kutumika kuendesha mfumo wa reli.

**Faida**

Reli za mwendokasi mara nyingi hupitia maeneo yenye mwanga wa kutosha wa jua, hasa katika nchi za Afrika kama Tanzania.

Paneli za sola husaidia kupunguza utegemezi wa mafuta ya kawaida.

**Changamoto**

Gharama za awali za kununua na kufunga paneli za sola zinaweza kuwa kubwa.

Matengenezo ya mara kwa mara yanahitajika kwa ufanisi wa muda mrefu.

**Mfumo wa Pamoja (Hybrid System)**

Ili kuongeza ufanisi, teknolojia hizi mbili " upepo na jua â€" zinaweza kutumika pamoja. Nishati inayozalishwa na turbine za upepo na paneli za sola inaweza kuhifadhiwa kwenye betri ndani ya treni au kutumwa moja kwa moja kwenye gridi ya taifa.

**Faida za Mradi Huu**

1. Kuchangia Nishati Jadidifu: Hii inasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**2. Kupunguza Gharama za Nishati:** Umeme unaozalishwa unaweza kutumika kuendesha treni, hivyo kupunguza gharama za kununua umeme kutoka vyanzo vya nje.

**3. Matumizi Bora ya Miundombinu:** Reli inaweza kutumika zaidi ya usafiri pekee kwa kuwa chanzo cha nishati kwa maeneo ya jirani.

Ingawa wazo hili halijatekelezwa moja kwa moja duniani, lina uwezekano mkubwa wa kubadilisha jinsi reli za mwendokasi zinavyofanya kazi, hasa katika nchi zinazotafuta suluhisho la nishati safi kama Tanzania. Kwa kuunganisha teknolojia ya upepo na jua, SGR inaweza kuwa sehemu ya maendeleo endelevu kwa kizazi kijacho.

Tanzania BORA



# Muendelezo Mkutano wa Nishati waipaisha Tanzania



BAADA ya Mkutano mwingine unaohusiana na masuala ya Nishati kufanikiwa mwaka jana hatimaye Tanzania inaendelea tena kuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa unaohusisha Marai wengi wa Afrika, Mawazi pamoja na wadau wa Maendeleo.

Mkutano huo ulianza jana Januari 27, 2025, ukiwakutanisha Mawaziri wa Nishati, Mawaziri wa Fedha, na wadau wa maendeleo ulianza kufanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere Jijini la Dar es Salaam, Tanzania.

Mkutano huu, unaojulikana kama 'Mission 300', unalenga kujadili mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati kwa watu milioni 300 Barani Afrika.

Viongozi mbalimbali, wakiwemo Wakuu wa Nchi za Afrika, wanahudhuria mkutano huu.

Mawaziri wa Nishati 60 wanashiriki katika mkutano huo ambao jana ulifunguliwa na Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko.

Mkutano mwingine wa kishitoria ulifanyika mwaka wa 2024, ukijulikana kama Mkutano wa Powering Africa wa EnergyNet ukiratibiwa huko Washington DC, USA, huku Kampuni tanzu ya Mara Holdings ikiazimia dhamira kushirikiana na nchi za Afrika Mashariki kwa kutia saini makubaliano makubwa na serikali ya Kenya, kuonyesha mwelekeo wa kile ambacho kinaweza kubadilisha mwenendo kwa eneo na uhalali wa kibiashara kwa Wazalishaji Nishati Binafsi (IPP) wengi.

Katika Mkutano wa Ushirikiano wa Nishati wa Afrika Mashariki (EA-ECS), uliofanyika Januari 29-30 jijini Arusha, Tanzania, umewaunganisha Wazalishaji Nishati Binafsi wa nishati za Afrika na wadau wa Uhandisi, Manunuzi, Ujenzi, na Fedha (EPCF) kutathimini uwezekano wa uwekezaji na uvumbuzi ulioanzishwa na makampuni muhimu kimkakati, ikijumuisha Vituo vya Data vya Afrika na iXAfrica.

Kiini cha ukuaji huu wa kikanda wa shughuli za uwekezaji ni Sekretarieti ya Afrika Mashariki (EAC), ambayo inawakutanisha wawekezaji na watengeneza sera pamoja na EnergyNet, kujikita katika "Utajiri wa Rasilimali. Upatikanaji wa Nishati. Fursa za Uwekezaji."

Kwa kuzingatia mafanikio ya mwaka jana, mkutano huu utakuza ushirikiano kote Afrika Mashariki, ukiangazia dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya ushirikiano wa kina wa kikanda na jukumu muhimu la kukuza viwanda na ushirikiano miongoni mwa wadau.

Ukiongozwa na Mawaziri kutoka nchi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki na watumiaji wakubwa wa nishati, kwa muda wa siku mbili, Mkutano wa Arusha ulijikita katika fursa kwa sekta binafsi, kuhimiza kuwepo kwa mseto wa nishati mbalimbali ili kudumisha ustahimilivu wa gridi ya taifa ili kusaidia ukuaji mkubwa wa viwanda, pamoja na uzalishaji wa umeme kwa matumizi ya kibiashara na biashara za viwandani.

"Nishati ni nguzo ya maendeleo na ukuaji na ni muhimu kwa utendaji kazi wa uchumi wa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki. Mkutano wa Ushirikiano wa Nishati wa Afrika Mashariki utatumika kama jukwaa bora la kuendeleza miradi na kuleta mabadiliko yanayoonekana katika sekta hiyo" amesema Mheshimiwa Andrea Malueth, Naibu Katibu Mkuu (Sekta ya Miundombinu, Uzalishaji, Jamii na Siasa), Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

EA-ECS itakaribisha wanasiasa na viongozi mashuhuri kutoka nchi zote za Afrika Mashariki na sekta zake za nishati. Wataungana na wakuzaji biashara wa sekta binafsi ambao wanatengeneza mustakabali wa mazingira ya nishati ya Afrika Mashariki, wakihudumia takriban watu milioni 500.

"Miaka kumi kutoka sasa, tabaka la kati la watu wa Afrika Mashariki litakuwa na uthabiti zaidi wa kazi, fursa zaidi, na kipato zaidi ukilinganisha na hapo awali. Reli mpya, viwanda, bandari na utalii vitalifanya eneo hili kuwa kivutio kikuu cha uwekezaji duniani, na kujitwalia nafasi hiyo kutoka eneo la Asia na Amerika Kusini," amesema Elisa Palmioli, Mtayarishaji, EnergyNet.



# Tangulia mwanamuziki Tabia Mwanjelwa

ILIKUWA ni mwishoni mwa mwaka 1982, bendi ya Orchestra Marquiz du Zaire ilikuwa ikirekodi katika kipindi cha Misakato kikirushwa na Redio ya Taifa enzi hizo ukiitwa RTD, Redio Tanzania Dar es Salaam.

Mtangazaji alikuwa Julius Nyaisanga, nilianza kusikia sauti zisizokuwa na asili ya bendi hiyo, maana niliwazoea waimbaji wa Marquis hata kwa sauti.

Nilizizoea sauti za akina Mbuya Makonga Adios, Mutombo Lufungula Audax, Nkulu Wabangoi na Mukumbule Parashi.

Hizi nilizokuwa nikizisikia sikuziekewa na zaidi sikuwa na taarifa kuwa bendi hiyo imeajiri mwimbaji wa kike.

Wimbo uliokuwa hewani ukiitwa 'Nabwela Mziko lya Zambia' uliimbwa kwa lugha ya Kinyanja ya nchini Zambia, nao ukazidi kunichanganya.

Pia kulikuwa na sauti nyingine mbili licha ya hii ya kike nazo sikuzielewa japokuwa moja nikahisi kama ilitokea katika bendi za Orchestra matimila na Tomatoma, sauti ya Kasaloo huwa haijifichi hata aimbe na wenzake 20 labda akiwemo pacha wake tu Kyanga Songa.

Nyaisanga ndiye aliyenituliza nafsi baada ya kumalizika wimbo na yeye akapitisha kama kitendawili pale alipoanza kusema...nanukuu.

" Huyo si Abeti Masikini na Wala siyo Miriam Makeba bali ni mwanamama Mzalendo wa Tanzania kutoka kitongoji cha Mwanjelwa mjini Mbeya, anaitwa Tabia Mwanjelwa.

Sentesi hiyo ndiyo iliyoliweka akilini mwangu jina hili moyoni mwangu, pia nikiendelea kushangaa uwezo wake mkubwa ilihali si mwanamuizki tuliyemsikia hapo nyuma.

Siku hiyo pia ndiyo nilipojua kuwa bendi hiyo imeongeza waimbaji wawili, Kasaloo Kyanga na Kasongo Mpinda walioletwa kuongeza nguvu ya kunogesha mtindo wa Ogelea piga mbizi.

Baadaye wanamuziki hawa wote walikuwa rafiki zangu, Kasaloo tukiishi majirani yeye akiwa Kinondoni nyuma ya ukumbi wa Vijana Hostel na Mimi Mwanyamala Komakoma jirani na Kasongo Mpinda na Asia Darwesh

Tabia nikakutana naye bendi ya Orchestra King Kiki akiimba na Lizzy Binti kutoka Afrika Kusini na Kapelembe Koko, aliniambia amejiujga na bendi hiyo Kwa kuwa inapiga muziki wa kimataifa na yeye ana ndoto ya kwenda kupiga muziki nchi za nje.

Sikumsikia tena hadi siku moja nilipmsikia kupitiua redio fulani akikanusha taarifa za kuzushiwa kifilo na kufafanua kwamba alikuwa fiti nchini Ujerumani, jhapo ndipo nilipojua kuwa dhababu hiyo imehamia Ughaibuni.

Mwaka 2017 tulikutana kwa mara ya mwisho nilipokuwa mmojawapo wa waandalizi wa tamasha lililoitwa Dimba Concert, yalikuwa ni maadhimisho ya gazeti la michezo maarufu nchini Dimba kujtimiza miaka 25 na kipimndi hicho mimi nikiwa Mhariri Mkuu.

Tabia hakuwa yule tena, alikuwa mtu mzima lakini bado alikuwa yumo katika dwimbwi la muziki, alipata nafasi ya kupanda jukwaani akiwa na gitaa lake na kutumbuiza kidogo, lakini kumbukumbu zile hakuwa na muda tena wa kuziweka bayana kutokana na mazingiza.

Nimepata taarifa ya kifo chake na kukipokea kwa uchungu kwa vile ni mwanamuziki ninayemfahamu na niliyezikubali kazi zake, Mewenyezi Mungu ampokee na kumpa hifadhi ya amani. Amen.



Tangulia mwanamuziki Tabia Mwanjelwa

UK. 15

Tanzania BORA MICHEZO

JUMANNE, JANUARI 28, 2025 TOVUTI: WWW.TANZANIABORA.CO.TZ

# Simba SC yapiga mkwara Ligi Kuu

NA MWANDISHI WETU

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya Robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikishol timu ya Simba imeweka wazi kuwa mkakati wake wa kuimarisha kikosi chake utaendelea na kwamba msimu ujao itatumia nguvu kubwa kufanya usajili.

Imeweka wazi kuwa usajili huo hautogusa wachezaji kutoka nje tu bali, utaaangalia mchezaji yeyote hata aliyekuwepo katika klabu kubwa za Tanzania iwe Simba au Yanga ambaye wataona ana viwango vya kuchezea Simba basi hawatasita kupiga hodi na kuondoka naye.

Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi wa Klabu hiyo Mohamed Dewji ametajwa kuwa ndiye aliyewapa idhini jipo lake la makocha kuangalia kwa makini na kwaa muda mrefu ili ikionekana kuna mchezaji mwenye viewango anayeweza kuisaidia timu yake basi ataarifiwe ili amalize kazi.

Kuna tetesi kuwa baadhi ya wachezaji mhumu watatu ndani ya kikosi cha Yanga wameonyesha nia ya kutamani kuichezea Simba kutokana na rekoidi yake na kucheza mechi za kimataifa na kufika mbali.



## Tizi Simba lazidi kukolea

NA MWANDISHI WETU

KOCHA Mkuu wa Simba Fadlu Davis amewapongeza wachezaji wake kwa kuongezeka kiwango cha Stamina na kuonyesha ukakamavu muda wote wa mchezo.

Kocha huyo licha ya timu yake kuichakaza Kilimanjaro Stars kwa jumla ya mabao 6-0, lakini amesema yeye alikuwa na kazi ya kufanya tathmini ya kila mchezaji kuangalia uwezo wake wa kuhimili dakika 90.

Pia ameeleza kufurahishwa na ushindi huo mnono wa michuano ya ASFA na kudai ndiyo dhamira ya timu yake msimu huu.

Kwa upande wake kiungo mkongwe katika kikosi hicho Mzamiru Yassin, amewasifu wachezaji wa Kilimanjaro akidai kuna baadhi ni wachezaji wazuri.

"Kuna mchezaji alivaa jezi namba 30 alikuwa mzuri sana na wengine kama watatu hivi" alisema.

Katika mchezo wa juzi Simba ilichezesha nyota wake ambao huko nyuma hawakupata nafasi nyingu za kucheza.

Gazeti hili hutolewa na Jamvi Media Group S.L.P 55151 Dar es Salaam.